THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021 **KISWAHILI**

(Kwa Watahiniwa Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 3 **Ijumaa, 21 Novemba 2014 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, B na D, swali **moja (1)** kutoka sehemu C na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu E. Swali la **15** ni lazima.

3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.

4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.

5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 10)

UFAHAMU

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:

   Rehema alifanya kazi ya uuzaji katika duka moja la vitambaa kwa mshahara wa shilingi laki moja na elfu ishirini. Mwenye duka limfurahia sana na kusema kuwa Rehema alikuwa na **uso wa biashara** na kama ilivyo mcheza kwao hutuzwa, basi mwezi uliofuata alimuongeza shilingi elfu ishirini katika mshahara wake. Mwezi mwingine uliofuata Rehema alituhumiwa kuwa ana **mkono mrefu**. Mwenye duka hakuona sababu ya kusubiri kilichopatikana kwa uso wa Rehema kiishie katika mkono wa Rehema. Kwa hali hiyo aliona bora waagane kwa salama.

   Baada ya muda mfupi alipata kazi katika kituo cha mafuta, kadhalika alionesha kuelewana vizuri sana na tajiri wake, kwani wanunuzi walizidi **mara dufu**. Lakini pia mwenye biashara alibaini kuwa palikuwa na **chemba** ya minong'ono isiyokwisha baina ya Rehema na wateja wa kiume. Rehema alibadili nguo hii na kuvaa ile, aliletwa kazini na kuchukuliwa kwa gari, hayo yalimfanya mwenye kituo cha mafuta **ashuku** kuwa anaibiwa mafuta yake, hapo pia Rehema alipewa ruhusa.

   Mungu hamtupi mja wake, Rehema alijaliwa kupata tena kazi, mara hii katika kampuni ya ushoni. Rehema alionekana mzuri mno hali iliyosababisha wivu na majungu yakaanza dhidi yake. Hakusubiri kuachishwa kazi mara hii alijiondoa mwenyewe. Aliamua kutafuta kazi za majumbani na alibahatika kupata kazi hiyo kwa **suriama** mmoja tajiri sana aliyekuwa anaishi katikati ya mji. Rehema kama ilivyo ada aliwajibika ipasavyo na alipata sifa mbele ya mwajiri wake.

   Maswali

   (a) Toa maana za maneno na vifungu vya maneno vifuatavyo kama vilivyotumika katika habari uliyosoma:
      (i) Uso wa biashara
      (ii) Mkono mrefu
      (iii) Mara dufu
      (iv) Chemba
      (v) Ashuku
      (vi) Suriama

   (b) Kwa kuzingatia habari uliyosoma usemi "hapo pia Rehema alipewa ruhusa" una maana ipi?

   (c) Kutokana na habari uliyosoma taja tabia mbili za Rehema zisizofaa kuigwa katika jamii.

2. Fupisha habari uliyosoma kwa maneno yasiyopungua sabini na tano (75) na yasiozidi themanini (80).

SEHEMU B (Alama 25)

SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Soma sentensi zifuatazo kisha kwa kila moja taja ni aina gani ya sentensi.
   (a) Mtoto alikuwa anakimbizana na wenzake.
   (b) Akisema ukweli atasamehewa.
   (c) Wanafunzi wanasoma kitabu na mwalimu anaandika ubaoni.
   (d) Kitabu kilichonunuliwa jana kitaletwa kesho darasani.
   (e) Ingelikuwa vyema tungelifahamiana leo.

4. Taja njia iliyotumika kuunda maneno yafuatayo:
   (a) Megawati
   (b) Tunasherehekea
   (c) Kifudifudi
   (d) Kasimawimbi
   (e) Nyau
   (f) Uzalishaji
   (g) Pekepeke
   (h) Pedeli
   (i) Ufagio
   (j) Kingamwili

5. Badilisha nomino zifuatazo ili ziwe vitenzi vilivyo katika kauli ya kutenda:
   (a) Hakimu
   (b) Msamaha
   (c) Msuluhishi
   (d) Kinyambuo
   (e) Uhamiaji
   (f) Mafichioni
   (g) Shuhuda
   (h) Masimulizi
   (i) Vichekesho
   (j) Upendo.

6. Tungo zifuatazo ni tata, toa maana mbili kwa kila tungo:
   (a) Wewe una ua?
   (b) Watoto wanamkimbilia Babu.
   (c) Kaka amenunua taa.
   (d) Kumbe ni tembo?
   (e) Sawa, sasa unaweza kuandaa sherehe.

7. Eleza maana ya vidahizo vifuatavyo kisha tunga sentensi moja kwa kila kidahizo.
   (a) Lambo
   (b) Sherasi
   (c) Makala
   (d) Pogoa
   (e) Umbeja

SEHEMU C (Alama 10)

UANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

8. Tumia kichwa cha habari "Faida nne za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za biashara nchini Tanzania" kuandika insha yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) na yasiyozidi mia nne (400).

9. Jifanye wewe ni diwani wa kata ya Kanyagatwende. Andika hotuba yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) na yasiyozidi mia nne (400) utakayoitoa kwa wananchi wako ukikemea tabia ya kuwachoma moto watu wanaosadikiwa kuwa ni wezi.

SEHEMU D (Alama 10)

MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali la **kumi (10)**

10. Kwa kutumia hoja nne na mifano, fafanua mchango wa vipindi mbalimbali vya redio katika kuimarisha lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

SEHEMU E (Alama 45)

FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **15** ni la lazima.

11. Kwa kutumia hoja tano, onesha jinsi maendeleo ya sayansi na teknolojia yanavyoboresha uhifadhi wa fasihi simulizi.

12. "Washairi wanasisitiza mshikamano miongoni mwa wanajamii." Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya diwani mbili zilizoorodheshwa.

13. "Wasanii wanafichua ukiukwaji wa haki za binadamu." Fafanua kauli hiyo kwa kutumia hoja tatu kutoka katika kila riwaya kati ya riwaya mbili zilizoorodheshwa.

14. “Uzembe huleta madhara katika jamii.” Thibitisha kauli hiyo kwa kuchagua wahusika watatu kutoka kila kitabu kati ya tamthiliya mbili zilizoorodheshwa. Kwa kila mhusika toa hoja moja inayoonesha madhara ya uzembe alioufanya.

15. Tunga dayalojia yenye maneno yasiyopungua mia mbili na hamsini (250) na yasiyozidi mia tatu (300) kuhusu maisha ya shule. Dayalojia hiyo ihusishe wanafunzi waitwao Jitahada na Maarifa.

ORODHA YA VITABU

Ushairi

Wasakatonge	-	M.S. Khatibu (DUP)
Malenga Wapya	-	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	-	T.A. Mvungi (EP & D.LTD)

Riwaya

Takadini	-	Ben J. Hanson (MBS)
Watoto wa Maman’tilie	-	E. Mbogo (H.P)
Joka la Mdimu	-	A.J.Safari (H.P.)

Tamthiliya

Orodha	-	Steve Reynolds (MA)
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe	-	E. Semzaba (ESC)
Kilio Chetu	-	Medical Aid Foundation (TPH)